# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

**03 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA THELATHINI NA NANE - TAREHE 03 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**484 MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya *X-Ray* mashine kwenye Vituo vya Afya Nkende na Kibumaye - Tarime.

**485 MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Chifutuka – Bahi.

**486 MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kujenga mifumo ya uvunaji maji ya mvua katika Shule zote nchini.

**487 MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Mabweni ya Wasichana ya Kidato cha Tano na Sita katika Shule za Kilindi na Mlongwema.

**488 MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaoendelea katika Mji wa Mpwapwa.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**489 MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Kada nyingine wanapewa madaraja mserereko kama ilivyo Kada ya Ualimu.

**490 MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Serikali isipeleke ajira kwenye ngazi ya Halmashauri ili kuweka uwiano wa nafasi katika kila Jimbo.

**WIZARA YA NISHATI:**

**491 MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme wa REA kwenye Vitongoji 37 ambavyo vipo gizani katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

## WIZARA YA KILIMO:

**492 MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa soko la Zao la Pareto.

**493 MHESHIMIWA MUHARAMI SHABAN MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika Jimbo la Bagamoyo hasa katika Mradi wa JICA.

## WIZARA YA MAJI:

**494 MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha miradi ya maji Kijiji cha Mangio, Mwaniko na Msangeni - Mwanga.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**495 MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itatatua migogoro ya mipaka ya Hifadhi Kata ya Mputa na Mchomoro - Namtumbo.

**WIZARA YA AFYA:**

**496 MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka Huduma za Afya bure kama ilivyo katika Elimu ya Msingi na Sekondari.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**497 MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itavitambua Vivutio vilivyopo Jimbo la Momba kama vile Nyayo za Mtu wa Kale, Nkanyama, Maporomoko ya Mfuso na Yala (Mpona).

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA AFYA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **03 JUNI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |